
TOLEO LA. 02

# Jarida la Ni Magufuli Tena

2020 - 2025

ALIAHIDI | AMETEKELEZA | APEWE TENA 5 | SEPTEMBA 2020

## MAGUFULI AFUNIKA IGUNGA, NZEGA



LIMEANDALIWA NA **TEAM MAGUFULI TENA**

# TAHARIRI

## TUSIKUBALI HOJA MUFILISI YA ACT WAZALENDO KUHUSU GESI

Wakati kampeni za kuwania Urais, Ubunge na Udiwani zikiendelea nchini, leo Chama cha ACT Wazalendo kimeendeleza utamaduni wake wa kupotosha kila juhudi zilizofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano katika kutekeleza miradi ya maendeleo ambayo kimsingi inasaidia kuleta maendeleo ya watu.

Leo katika uzinduzi rasmi wa Chama hicho ulifanyika Lindi Mjini na kukosa mvuto huku kukiwa na mwitikio mdogo wa wananchi, amesikika Kiongozi Mkuu wa Chama, Zitto Kabwe amejaribu kuwahadaa wananchi wachache waliohudhuriauzinduzi huo kwa kusema kuwa gesi inayopatikana haijawanufaisha wananchi wa Kanda ya Kusini na watanzania kwa ujumla.

Tunapenda kumkumbusha Zitto kuwa Gesi imekuwa na manufaa makubwa ambapo gesi inayopatikana imewezesha kuzalisha umeme katika mitambo ya Kinyerezi I, Kinyerezi I-Extension na Kinyerezi II ambapo hadi kufikia Disemba mwakahuu,jumla ya megawati 583.22 zitakuwa zimeingizwa katika gridi ya Taifa ambazo zinatumika nchi nzima ikiwemo mikoa ya Lindi na Mtwara.

Tunawafahamisha tu Zitto na ACT Wazalendo kwamba gesi asilia kwa sasa imeunganishwa katika kiwanda cha Saruji cha Dangote ambacho kimetoa ajira lukuki kwa wananchi wa Lindi na Mtwara na watanzania kwa ujumla na pia kuongeza upatikanaji wa saruji nchini.

Mpaka sas TPDC imesambaza gesi asilia kwa nyumba zaidi ya 500 na viwanda 48 katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Dar es Salaam na Pwani, magari zaidi ya 400 yanatumia gesi asilia. Hii ni faida nyingine ambayo ACT Wazalendo hawaiona walakuonesha uzalando.

Serikali ikekamilisha ujenzi wa miundombinu ya usambaji gesi (trunk lines) yenye urefu wa kilometa 17 na uwezo wa kuunganisha wateja zaidi 3000 wa majumbani katika mkoa wa Mtwara, kilometa 18 zenye uwezo wa kuunganisha wateja zaidi ya 10,000 katika mkoa wa Dar es Salaam na kilometa sita zenye uwezo wa kuunganisha zaidi ya viwanda 20 katika mkoa wa Pwani.

Kwa upande wa mradi wa Gesi ya Liquefied NaturalGas (LNG) unaotarajiwa kutekelezwa katika eneo la Likong'o, mkoani Lindi, Serikali imelipa fidia zaidi ya shilingi bilioni tano ili kupisha mradi ambao utawezesha kusafirisha na kuuza gesi nje ya nchi na fedha zinazopatikana zinatumika kuwaletea wananchi maendeleo.

Tunapenda kuwakumbusha na kuwasisitiza wananchi kuwa makini na wanasiasa wachumiatumbo ambao ajenda yao kubwa ni kupotosha, kutukana na kuwahadaa wapiga kura badala ya kuuza Sera. Tutambue kwamba Urais sio mahali pa kufanyia majaribio. Uongozi unahitaji mtu makini, mkweli na mchapa kazi.



# IGUNGA, NZEGA WAMPA MITANO TENA MAGUFULI

Na Mwandishi Wetu, **NZEGA**



Umati mkubwa watu uliojitokeza katika Wilaya za Igunga na Nzega kumsikiliza Rais Magufuli umedhihirisha uimara wa CCM na kinakubalika katika Wilaya hizo.

Rais Magufuli amewashukuru wananchi katika Wilaya hizo kuwaahidi kuwa ataendelea kuwa mtumishi wao na kujitoa sadaka kuwatumikia wanyonge na wananchi wote bila kujali itikadi za vyama vyao.

"Kazi yangu mimi na Serikali ninayoiongoza ni sadaka kwa watanzania walio wanyonge. Nawaambia ndugu zangu wa Nzega, matusi niyapate lakini nyinyi mpate maendeleo ya kweli. Najua wanaotukana hawapendi mambo makubwa ninayofanya," anaeleza Magufuli.

Dkt. Maguli ambae anaamini katika kuwatumikia wananchi wote bila kujali itikadi zao za vyama, amesema miradi mingi imetekelezwa ikiwemo ya barabara za Nzega na Tabora Mjini kwa kiwango cha lami, Tabora-Manyoni ambayo imekia kilometa 20 kukamilika, Tabora-Kigoma na Tabora-Mpanda, pamoja na vituo vya afya ambapo kwa ujumla wake zinanufaisha wananchi kutoka vyama vyte.

# RAIS MAGUFULI: MCHAGUENI AHMED SALUM, AMEKUWA AKIWATETEA SANA BUNGENI

Na Mwandishi Wetu, **Tinde - SHINYANGA**




Rais Dkt. John Pombe Magufuli ambaye pia ni Mgombe Urais kwa tiketi ya CCM, amewaomba wananchi wa Tinde na jimbo la Solwa mkoani Shinyanga kumchagua Bw. Ahmed Salum kuwa mbunge wa jimbo hilo kwa sababu ni mchapa kazi na amekuwa mstari wa mbele katika kuwatetea wananchi wake.

Mhe. Magufuli ametoa rai hiyo leo Septemba 2, 2020 aliposima eneo la Tinde mkoani Shinyanga kuongea na wananchi wa eno hilo na maeneo ya jirani katika jimbo la Solwa.

"Mbunge wenu huyu Ahmed Salum amekuwa akiwatetea sana na ndiyealiyekuwa mstari wa mbele kuwatetea patia Chama ushindi wa kishindo.

wachimbaji madini wadogo wa eneo hili. Aliwatete mpaka nikamtuma Biteko (Dotto Biteko-Waziri wa Madini)," alieleza Magufuli.

Rais Magufuli amewataka wananchi na wana CCM wa jimbo la Solwa kuendeleza umoja na mshikamano na kutolea mfano wa aliyekuwa Mbunge wa Msalala, Ezekiel Maiga na Sinyanga Mjini, Stephen Masele ambao licha ya kutopitishwa na Chama kugombea Ubunge lakini wamefika Tinde kuwaunga mkono wagombea ili kuki

"Mbunge wenu huyu Ahmed Salum amekuwa akiwatetea sana na ndiye aliyekuwa mstari wa mbele kuwatetea wachimbaji madini wadogo wa eneo hili. Aliwatete mpaka nikamtuma Biteko (Dotto Biteko-Waziri wa Madini)," alieleza Magufuli.

Rais Magufuli amewataka wananchi na wana CCM wa jimbo la Solwa kuendeleza umoja na mshikamano na kutolea mfano wa aliyekuwa Mbunge wa Msalala, Ezekiel Maiga na Sinyanga Mjini, Stephen Masele ambao licha ya kutopitishwa na Chama kugombea Ubunge lakini wamefika Tinde kuwaunga mkono wagombea ili kukipatia Chama ushindi wa kishindo.

Amesema katika Awamu ya pili ya Serikali yake, wananchi wa Tinde watanufaika na maji kutoka Ziwa Victoria ambapo yatasambazwa kutoka bomba kuu kuingia kwa wananchi.

Rais Magufuli amewasihi wananchi kumpa kura za kishindo yeye pamoja na wagombea Ubunge na Udiwani wa CCM ili watekeleza ahadi za Chama kwa ufanisi zikiwemo huduma za afya na maji.

'Nileteeni Wabunge wa CCM na hapa Solwa mniletee Amemed. Mkinichagulia Wabunge wa CCM au Maiwani ninauwezo wa kumbana," aliwaeleza wananchi huku akiwaaidi kutatua changamoto ya madaktari na manesi katika eneo hilo.



# WANANCHI MANYARA WAAHIDI KURA ZOTE KWA MAGUFULI

Na Mwandishi Wetu, **MANYARA**




Wananchi wa Mkoa wa Manyara wameahidi kumuunga mkono kwa asilimia 100 mgombea Urais wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Dkt. John Pombe Magufuli, Wabunge na Madiwani katika uchaguzi mkuu wa Oktoba 2020.

Wakizungumza katika mahojiano maalum leo eneo la Magugu, mkoa wa Manyara, Bw. Joseph Ami amesema kuwa wameridhishwa na utekelezaji wa ilani ya CCM katika kipindi cha miaka mitano iliyopita na ahadi zilizotolewa kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

"Mgombea wa CCM kwa nafasi ya Urais na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli ametufuta machozi na kutuwezesha kutembea kifua mbele. Leo tuna vituo vya afya, zahanati, miradi ya maji, elimu na miundombinu," alieleza Ami.

Akifafanua anasema kwa sasa elimu bure imejenga imani kubwa kwa CCM mbele ya wananchi kwani imetoa fursa ya watoto wa wanyonge kupata elimu ambayo hapo awali walikuwa haipati.

Kwa upande wake John Antony mkazi wa Magugu anasema kuwa hakuna sababu ya wananchi wa mkoa huo kuinyima kura CCM kwa kuwa imeahidi na kutekeleza kama ahadi zake na inayo mipango inayopimika ikilenga kuwakomboa wananchi kiuchumi.

Aliongeza kuwa wananchi hasa wakulima hawabugudhiwi kupitia tozo mbalimbali hali inayowapa wananchi fursa ya kuchangia maendeleo yao na Taifa kwa ujumla. Serikali ya Awamu ya Tano ilifuta zaidi ya tozo 114 katika mazao kumpa unafuu mkulima.

Kwa upande wake mbunge aliyemaliza muda wake, Jituson Patel amesema kuwa ana uhakika kuwa mkoa huo utaongoza kwa wananchi wake kupiga kura za ndio kwa CCM.





# MAGUFULI AMALIZA UTATA FAIDA ZA NDEGE AKIWA MANYONI

Na Mwandishi Wetu, **Manyoni - SINGIDA**

Hoja dhaifu ya wapinzani kupinga maendeleo ya vitu kama vile ununuzi wa ndege ambayo imekuwa ikipotoshwa na wapinga maendeleo, leo imezimishwa na Mgombea wa CCM, Dkt. John Pombe Magufuli kwa maneno rahisi sana na wananchi kumuelewa.

Akiwa Wilani Manyoni, Rais magufuli ameongea na maelfu ya wananchi waliokusanyika kumsikiliza amapo aliwauliza kama dawa za hospitali zinazotengenezwa Ulaya huwa zinaletwa na pikipiki maarufu kama bodaboda, lakini wananchi walionesha ulewa mkubwa kuhusu uwekezaji wa Serikali kwa kuunga mkono ununuzinwa ndege kwani zinarahisisha usafiri wa watu na bidha kama dawa mabzo zina manufaa kwa wananchi.

“Katika miaka Mitano hii tumewajengea shule, vituo vya afya, maji, umeme mpaka mandege tumeleta, sasa nasikia watu wanawadanganya eti ndege zinawasaidia nini hapa Manyoni.

Sasa niwaulize hivi hapa Manyoni dawa za kuwatibu zinazotoka Ulaya zinaletwa na ndege au pikipiki kuja nchini?,” aliuliza Rais Magufuli na wananchi kwa sauti kuu walijibu kwamba zinaletwa na ndege.

Rais Magufuli huku akishangiliwa na maelfu ya wazee, vijana na watoto waliofika kumsikiliza, pamoja na ahadi zingine alieleza Serikali yake itaendelea kununua ndege zaidi katika kwa kuwa ni uwekezaji na faida inayopatikana kutokana na uendeshaji wa ndege hizo inatumika kutekeleza miraji inayowanufaisha wananchi.




Air Tanzania
The Wings of Kilimanjaro
anzania.co.tz


Air Tanzania






Air Tanzania




Air Tanzania


Air Tanzania




Twiga

# MAGUFULI AWASHA MOTO SINGIDA

Na Mwandishi Wetu, **SINGIDA**




Baada ya kuzindua kwa kishindo kampeni za Urais, Ubunge na Udiwani katika Uwanja wa Jamhuri Jijini Dodoma Jumamosi iliyopita, Mgombe Urais kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM) Dkt. John Pombe Magufuli leo ameendelea mikutano yake katika mkoa wa Singida na kupokelewa na maelfu wa wananchi.

Akiwa mkoani Singida, Rais Magufuli amepokelewa kwa shangwe na wananchi waliokuwa na shauku ya kumuona na kumsikiliza Rais Magufuli ambaye amekuwa ni lulu kwa watanzania kutokana na mafanikio makubwa katika kutekeleza ahadi za kuwaletea maendeleo.

yanamshangaa. Ninashukuru na wala sijutii kufunga safari kutoka Mkalama kwa sababu huyu ni Rais asiyetaka mchezo katika kazi na siku zote amekuwa akitekeleza ahadi," anaeleza Joseph Lameck (49) kutoka Mkalama.

Nae Eliakim Maliyamungu (45) amabye ni mfanyabiashara wa mazao anaishukuru Serikali ya Awamu ya Tano kwa kujenga miundombinu wezeshi ambayo imeigeuza Singida kuwa na muonekano wa tofauti na unaopendeza tofauti na miaka ya nyuma.

"Singida ya sasa siyo ile ya miaka ya nyuma. Miundombinu ya barabara zenye taa, umeme na huduma za afya imekuwa msaada mkubwa sana kwa sisi wafanyabiashara," anaeleza Eliakim.



Bi. Mariam Mussa (42) mama wa watoto mapacha ambaye alikuwa amejipumzisha chini ya mti pembeni ya viwanja vya Bombardier sambamba na mapacha wake anasema maboresho katika vituo vya afya vimeokoa maisha yake na wanae baada ya kulazimika kufanyiwa upasuaji katika Kituo cha Afya cha Karume kilichopo Singida mjini.

"Bila juhudi za Magufuli kutujali wakinamama pengine mimi au wanangu mmoja wapo angekuwa amekufa. Nilienda kujifungua lakini ilishindikana kwa njia ya kawaida na nilikuwa tayari nimechoka sana lakini namshukuru sana huyu Rais na ndio maana nimeona tu nije hata nimuone kwa mbali na kumsikiliza kwa sababu najua atatuletea maendeleo zaidi," anaeleza Bi. Mariam.
Rais Magufuli anatarajiwa kuendelea na kampeni kesho Septemba 1, 2020 katika mkoa wa Shinyanga.





# 5 ZA UTEKELEZAJI WA DKT. JOHN POMBE MAGUFULI MKOA WA SINGIDA

1. TUMETUMIA SHILINGI BILIONI 470.4 KUTEKELEZA MIRADI YA MAENDELEO KATIKA MKOA WA SINGIDA.

2. TUMEJENGA VITUO VYA AFYA VILIVYOWEZESHA AKINAMA 730 KUFANYIWA UPASUAJI NA KUSAIDIA KUOKOA MAISHA YAO NA WATOTO.

3. TUMETUMIA SHILINGI BILIONI 52.6 KUJENGA MIUNDOMBINU YA SHULE YAKIWEMO MADARASA, MAABARA NA MIUNDOMBINU MINGINE NA SHILINGI BILIONI 310 KUJENGA MIUNDOMBINU WEZESHI YA KIUCHUMI.

4. TUMETUMIA BILIONI 27.2 KUTEKELEZA MIRADI YA MAJI IPATAYO 66 NA BILIONI 17 KUJENGA BARABARA ZA SINGIDA MJINI NA KUZIWEKEA TAA.

5. TUMEJENGA DARAJA LA SIBITI NA KUONDOA KERO YA WANANCHI KUSHINDWA KUVUKA MTO SIBITI HASA WAKATI WA MASIKA.

# 5 AHADI TANO ZA DKT. JOHN POMBE MAGUFULI KWA WANA-SINGIDA

1. AJIRA MILIONI 6 ZIMEZALISHWA KATIKA KIPINDI CHA MIAKA MITANO NA SASA MIAKA MITANO IJAYO TUTAZALISHA AJIRA MILIONI 8.

2. HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA SINGIDA IKO HATUA ZA MWISHO KUKAMILIKA IKIWA NI HATUA MOJAWAPO YA KUBORESHA SEKTA YA AFYA.

3. UJENZI WA BARABARA YA CHAYA SINGIDA HADI TABORA IMEBAKI KM 20 KUKAMILIKA.

4. TUMEFIKISHA UMEME KATIKA VIJIJI 9,570 KATIKA KIPINDI CHA MIAKA MIWILI IJAYO TUTAMALIZIA KIFIKISHA UMEME KATIKA VIJIJI 2,600 VILIVYOBAKIA.

5. NIKO HAPA KWA UNYENYEKEVU MKUBWA KUOMBA KURA ZA VYAMA VYOTE KWA SABABU MAENDELEO HAYANA CHAMA.



# MAMA SAMIA SULUHU AREJESHA MATUMAINI YA WANA-MIKUMI, GAIRO MKOANI MOROGORO

- ***UZALISHAJI MIWA KUONGEZEKA KUTOKA TANI 130,000 HADI 170,000***
- ***KUPANUA SOKO LA MIWA, AJIRA***

Na Mwandishi Wetu, **Mikumi - MOROGORO**

Mgombea Mwenza wa Urais kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM), Samia Suluhu Hassan amesema endapo wananchi watamchagua Dkt. John Pombe Magufuli, watahakikisha Serikali ya CCM inaendelea kusimamia uzalishaji wa sukari katika kiwanda cha Kilombero kutoka tani 130,000 ya sasa hadi kufikia tani 170,000 na kupanua soko la kilimo cha miwa litakalowanufaisha Wakulima wa Mkoa huo.

Ameyasema hayo wakati wa mkutano na wananchi wa Gairo, Dumila na Mikumi Mkoani Morogoro wakati akihutubia kwenye mikutano ya Kampeni kumnadi mgombea wa Urais kupitia CCM Dkt. John Pombe Magufuli, Septemba 1, 2020.

"Ndugu zangu wa Morogoro, kama mlivyoona katika kipindi cha miaka mitano iliyopita Serikali yenu sikivu ya CCM inayoongozwa na Dkt. Magufuli, imefanya mambo mengi, tumeleta tija kwenye kilimo cha miwa na uzalishaji mzuri wa sukari, tutaendelea kusimamia hili.

"Tuchagueni CCM, mchagueni Mbunge wa CCM, chagueni madiwani na Rais Magufuli. Uchaguzi uliopita mlifanya makosa Jimbo hili la Mikumi kwa kutomchagua Mbunge wa CCM, sasa msirudie kosa hilo tena, mkimchagua Magufuli na viongozi wa CCM tutafanya haya yote pamoja," alieleza Mama Samia baada ya mgombea Ubunge Jimbo la Mikumi kumweleza juu ya changamoto ya kukosa soko la miwa.

Ameeleza kuwa katika kuhakikisha wakazi wa Mikumi wanapata maendeleo ya kijamii, Serikali ilitoa zaidi ya shilingi bilioni 10 kwa ajili ya ujenzi wa miradimbalimbali hiyo ikiwepo shule, hospital na miundombinu mingine ambapo tayari hospital ya kisasa iliyotumia shilingi milioni 400 imejengwa.

Aidha Mhe. Samia amesema Serikali inaimarisha ujenzi wa barabara kumi za mkoa huo kwa kwango cha lami ikiwepo barabara ya Kilosa-Dumila kilomita 18, Lupilo-Kitanda Kilomita 296 na Kilosa-Mikumi Kilomita 72.8.

Kwa upande wa huduma za usafirishaji wa reli alisema watahakikisha wanafufua reli ya kati inayopita Kilosa, Mikumi hadi Ifakara Mkoani Morogoro kama ilivyokuwa kwa Mikoa ya Kanda ya kaskazini ambao sasa wanafurahia huduma hizo walizozikosa miaka zaidi ya 30 illiyopita.



# MWIGULU ATAKA SINGIDA KUMCHAGUA TENA MAGUFULI 2020

- *ASEMA CHADEMA WAMECHUKUA 'ADVANCE' KWA MABEBERU*
- *NI HATARI KUWAKABIDHI NCHI WAPINZANI*

Na Mwandishi Wetu, **SINGIDA**

5.




"Rais Magufuli ameonesha uzalendo kwa watanzania amehangaika na watanzania kuwaletea maendeleo. Hospitali, vituo vya afya, maji, barabara, umeme vijijini na mengine mengi yametekelezwa kwa kipindi kifupi cha miaka mitano," anaeleza Mwigulu Nchemba kuwaomba wananchi wa Singida kumchagua Rais mzalendo badala ya kufanya majaribio kwa katika kuongoa nchi.

Nchemba ambae anagombea Ubunge jimbo la Singida Magharibi kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi (CCM), amefichua siri kuwa baadhi ya vyama vya upinzani vimekuwa vikishirikiana na mabeberu katika kuihujumu nchi na hivyo kuchagua upinzania ni sawa na kuiweka nchi rehani.

“Wapinzani wamekuwa wakishirikiana na mabeberu kuihujumu nchi yetu na si ajabu wengine watakuwa tayari wamepewa hela ya utangulizi (advance) hivyo ni hatari nchi yetu kuuzwa, na ndio maana nawaomba wana-Singida wote kumchagua Rais Magufuli ambaye ameonesha uzalendo na amejitoa kwa ajili ya watanzania,” anaeleza.

Mwigulu Nchemba alitumia fursa hiyo kuwaomba wananchi wote wa Jimbo la Iramba Magharibi kumpa kura za ndiyo katika nafasi ya Ubunge katika Jimbo hilo ili aendeleze mageuzi makubwa na maendeleo yaliyotekelezwa katika jimbo hilo.



# MEMBE AAHIDI KUREJESHA KANGOMBA UNUNUZI WA KOROSHO

- ***NI MFUMO KANDAMIZI UNAOMNYONYA MKULIMA***

Na Mwandishi Wetu, **LINDI**



Unaweza kusema ndugu Bernard Camilius Membe mgombea Urais wa ACT Wazalendo amelogwa au amekosa uzalendo baada ya kutangaza kurejesha mfumo wa dhuruma wa ununuzi wa Korosho maarufu kama Kangomba.

Bila aibu wa kupepesa macho, Membe ametamka kurejesha mfumo wa hovyo na unaoendeleza umasikini kwa wakulima, wakati wa uzinduzi wa kampeni za Chama hicho leo Septemba 1, 2020 mkoani Lindi.

Kangomba ni mfumo wa ununuzi wa korosho ambapo mnunuzi au wakala anatumia shida aliyonayo mkulima kwa kununua maua yaliyostawi vizuri katika mikorosho au kumkopesha mkulima fedha kidogo kidogo kutokana na shida aliyonayo na wakati mwingine kununua korosjo kwa bei ndogo na hivyo mkulima kupata fedha ndogo tofauti na mkulima akisubiri korosho zikomae ili aziuze kwa bei nzuri.

Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Rais Dkt. John Pombe Magufuli iliingiliankati na kuwaondoa wafanyabiashara wanyonyaji wanaotumia mfumowa kangomba na kumsaidia mkulima kuuza korosho kwa bei nzuri yenye faida.

Pamoja na kujaribu kuwashawishi waikubali Kangomba, wananchi waliohudhuria kampeni hiyo walionekana kuguna na kutoikubali sera hiyo kwa kuwa wanajua namna mfumo huo ulivyokuwa ukiwamasikinisha.


"Huyu Membe ni kama vile hajawahi kuwa Waziri au labda ana ajenda ya siri. Haiwezekani anataka kuturudisha kwenye mfumo wa Kangomba ambao ulikuwa unatufanya mwisho wa mavuno tusiwe na pesa mfukoni wala korosho shambani," alieleza Mzee Mohamed Maridadi (59) huku akionesha kupoteza matumaini kwa mgombea huyo wa Urais.

Katika uzinduzi huo wa kampeni, Membe ambaye alishindwa kupeleka maendeleo katika Jimbo la Mtama kwa kipindi chote alichokuwa Mbunge wa Jimbo hilo, yeye pamoja na viongozi wa Chama hicho akiwemo Kiongozi Mkuu wa Chama, Zitto Kabwe na Mwenyekiti, Maalim Seif Sharif Hamad walishindwa kunadi Sera na badala yake walitoa kauli za kulaumu na kupinga maendeleo na hivyo kuwafanya wananchi wasielewe kitu hasa Chama hicho kinasimamia.



# Jarida la Ni Magufuli Tena

2020 - 2025



LIMEANDALIWA NA **TEAM MAGUFULI TENA**